**Msururu wa Upotofu na Udanganyifu**
**Kuweka wazi yanayotatiza - Toleo la (4)**

Kuswahihisha fahamu juu ya

# Al-Walaa' na Al-Baraa'

Abd-ul-Fattaah bin Swaleh Qudeish Al-Yaafiey

SANAD

Sw

Deviance_Isssue_07_Sw.indd 1 13/11/17 13:41

بسم الله الرحمن الرحيم

بسم الله الرحمن الرحيم

Kila jinsi ya sifa njema ni za Allah mlezi wa viumbe wote, rehma na amani zimshukiye bwana wetu Muhammad na jamaa zake na swahaba zake na aliewafuata wao vyema hadi siku ya Qiyamah, na baada ya hayo:

Hakika neno Al-Walaa’ wa Al-Baraa’[1]ni neno la kuzuka hivi zama za mwisho mwisho, wala halikujulikana kwa waliotangulia wala kwa wanavyuoni kwa karne nyengi zilizopita, wala halikukomea jambo lenyewe kua ni neon tu, bali kwa neno hili kumepatikana mashakil mangapi ndani ya Ummah, ni damu ngapi zimemwagwa chini ya neno la Al-Walaa’ wa Al-Barraa’ na ni hishma ngapi zilizovunjwa chini ya neno Al-Walaa’ wa Al-Baraa’ na ni mali mangapi yamenyakuliwa chini ya neno Al-Walaa’ wa Al-Baraa’ na ni fahamu ngapi zilizopinduliwa chini ya neno Al-Walaa wa Al-Baraa’ na ni maana mangapi yameharibiwa chini ya neno Al-Walaa’ wa Al-Baraa’.

## Hakuna *Baraa’* Na Muislamu

Kinachopasa juu ya Muislamu ni kumpenda na kumnusuru na kumfanya rafiki na ndugu wala hakuna uchukivu au utengano au uaduwi, Amesema Allah aliyetukuka: ﴿Na waumini wa kiume na wakike baadhi yao ni marafiki ya baadhi﴾ na amesema Aliyetukuka: ﴿Hakika waumini ni ndugu﴾ na amesema ﷺ: (Muumini kwa muumini ni kama jengo)[2] na amesema ﷺ: (Mfano wa waumini katika kupendana kwao na kusikitikiana kwao na kuhurumiana kwao ni kama mfano wa muwili mmoja)[3].

Na kukisemwa: Vp kwa muislamu aswi[4] na mzushi? Kutasemwa: Hakika twachukia na kujiepusha na amali yake inayokhalifu shariya, sio dhati yake ambayo imebeba (La ilaha illa-Allah) kwa aya zilizotanguliya na Hadithi na mfano wa hizo, na kwa neno lake

1 Walaa’ ni kujikurubisha na mtu kiurafiki na Baraa’ ni kujiepusha na mtu kwa uaduwi.
2 Imeafikiwa na Bukhari na Muslim, Kwa mana wameikubali kuwa ni Hadithi swahihi.
3 Imeafikiwa na Bukhari na Muslim, Kwa mana wameikubali kuwa ni Hadithi swahihi.
4 Anayemuaswi Allah ﷻ kwa kufanya mambo kinyume na shariya.



Deviance_Isssue_07_Sw.indd 2-3 13/11/17 13:41

Allah alietukuka: ﴿Na shukisha bawa lako[1] kwa waumini waliokufuata (215) hivo wakikuasi basi sema mimi najiepusha na munayoyafanya (216)﴾ wala hakusema: (Basi sema mimi najitenga na nyinyi ) na katika hadithi ni kua Mtumi ﷺ alisema Khalid alipokosea: (Ewe Mola mimi najiepusha kwako kutokana na aliyofanya Khalid)[2] wala hakusema: mimi najiepusha kwako kutokana na Khalid. Na katika Musannaf Abd-ur-Razzaaq (11/18) (kutoka kwa Abi Qalabah kuwa Ab-id-Dardaa' alimpitia mtu aliyefanya dhambi watu wakawa wanamtukana, akasema: Je mwaonaje lau mungempata katika shimo je hamungemtowa? Wakasema: bali tungemtowa, akasema: basi musimtukane ndugu yenu, na mumshukuru Allah ambae amewaafu, wakasema: Je humchukii? Akasema: Hakika nachukiya amali yake, hivo akiiwacha basi ni ndugu yangu).

## Kuamiliyana Na Muislamu Anayeaswi[3]

Katika Swahihi za Bukhari (6/2489) kutoka kwa Omar Bin Khatwaab Allah awe radhi naye: Kuwa kuna mtu zama za Mtumi ﷺ alikuwa jina lake ni Abdallah, na alikuwa amebandikwa jina punda, na alikuwa akimchekesha Mjumbe wa Allah ﷺ naye ﷺ amemchapa kwa kunwa tembo, akaletewa siku moja akaamrisha achapwe, mmoja kati ya watu akasema: Ewe Mola mlaani ni sana mara ngapi analetwa? Mtumi ﷺ akasema: ( Musimlaani kwani wallahi sijui ila nikuwa anampenda Allah na Mjumbe wake).

Na katika riwaya nyengine ya Bukhari alisema Mtumi ﷺ: (Musiseme hivo, musimsaidiye shetwani juu yake) na katika Musnad ya Imam Ahmad (2/299) alisema Mtumi ﷺ: (Musiseme hivo, musimsaidiye shetwani juu yake, lakini semeni: Allah akurehemu).
Peleleza pamoja na mimi vp Mtumi ﷺ alikasirika na njiya hini katika kuamiliyana na wanaoaswi na akawambiya maswahaba: (Musimlaani kwani wallahi sijui ila nikuwa anampenda Allah na Mjumbe wake) (Musiseme hivo, musimsaidiye shetwani juu yake) (lakini semeni: Allah akurehemu). Hakika ilikuwa njiya ya kuamiliyana kwake Mtumi ﷺ pamoja na wanaoaswi ni kuhimiza na kukuza pande za kheri ambazo wako nazo, kwani huyu swahaba amelewa lakini Mtumi ﷺ amewatajiya maswahaba zake -na huyo mtu yuwasikiya-

1 Bawa lako kwa mana ya nguvu zako, yani wahurumie na uamiliane nao kiupole.
2 Surat-us-Shuaraa' Ayah 215 - 216.
3 Anayemuaswi Allah ﷻ ni yule anayefanya mambo kinyume na shariya.



kuwa anampenda Allah na Mtumi wake, ili awafundishe mwanzo vp waamiliyane na wanaoaswi, na pili ili mfumo huo unapelekeya zaidi kuacha anayeaswi maaswiya yake, kwani mkazo na ukali aghalabu unapelekeya kwenye ukaidi, na tukifaradhia kukapatikana kutekeleza kwa mwenye kukhalifu kwa ajili ya mkazo basi huwa ni kutekeleza kwa juu juu wala hakutoki moyoni, na hakika amesema Mtumi ﷺ: (Upole hauingizwi kwenye kitu ila hukipamba wala hautolewi kwenye kitu ila hukichukiza)[1] na amesema ﷺ: (Sihalali kwa muislamu kumgura ndugu yake [muisilamu] zaidi ya [siku]tatu)[<?>]

## Urafiki Na Uaduwi Juu Ya Misingi Ya Misamayati Midogo Mdogo

Taamali na mimi neno lake Allah aliyetukuka: ﴿ Hakika waumini ni ndugu basi suluhisheni kati ya ndugu zenu ﴾ ﴿Na waumini wa kiume na wakike baadhi yao ni marafiki ya baadhi ﴾ na mfano wa Ayah hizo, na taamali na mimi Hadithi: (Muislamu ni ndugu wa muislamu, hamdhulumu wala hamtozi nusura wala hamdharau)[<?>] (Kila muislamu kwa muislamu ni haramu damu yake na mali yake na hishma yake) na mfano wa Hadithi hizo.

Je umeona katika Ayah hizo na Hadithi upambanuzi baina ya muisilamu na muisilamu kwa misingi ya mategemezi ya kimadhehebu ama kivikundi ama kisehemu? Kalla wallahi, bali mategemezi ya urafiki na mapenzi na kunusuriana ni kuthubutu na uisilamu, hivo atakaethubutu na uislamu basi anafaa kupendwa na kunusuriwa itakavokuwa madhehebu yake au kikundi chake au nchi yake, amesema Mtumi ﷺ: (Atakaeshuhudia kuwa hakuna mungu ila ni Allah na akalekea kibla chetu na akaswali swala yetu na akala vichinjwa vyetu basi huyo ni muislamu anastahiki wanayostahiki waislamu na ni juu yake yaliyojuu ya waislamu)[<?>].
Lakini hali ilivyo iko mbali kila umbali na hayo, hivo utapata urafiki na uaduwi hivi sasa -na kwa zama zirefu- umesimama juu ya msingi wa kuwemo kwenye madhehebu au kikundi au mahali.

1 Hadithi hini imepokewa na Muslim.
2 Imeafikiwa na Bukhari na Muslim, Kwa mana wameikubali kuwa ni Hadithi swahihi.
3 Hadithi hini imepokewa na Muslim.
4 Hadithi hini imepokewa na Bukhari.



Deviance_Isssue_07_Sw.indd 4-5 13/11/17 13:41

## Je Kujiepusha Na Ukafiri Kwalazimu Muamala Mbaya?

Baadhi ya watu wanadhani kuwa kujiepusha na ukafiri na makafiri kunalazimu tuamiliane na wao kwa tabiya mbaya na kivita na ugumu na mkazo na kutokuwa laini na upole na kutokuwa na sikitiko na huruma, na hunu ni ufahamu wa makosa kinyume na Qur'ani takatifu na Hadithi tukufu, na mbora anaepigiwa mfano wa maana ya Muwaalaah na Mu'adaah[1] ni yule ambaye juu yake zimeteremka Ayah hizo rehma na amani ziwe juu yake na jamaa zake, hivo basi acha tufanye maonesho ya baadhi ya Ayah na Hadithi katika kuamiliyana pamoja na wasiowaisilamu wenye maudhi na vita licha ya waliosalama:

Kutoka kwenye Qur'ani takatifu Allah alimwambiya Nabii Musa na Haaruun amani iwe juu yao: ﴿Nendeni kwa firauni hakika yeye amepita mipaka (43) basi mumzungumziye maneno laini huenda akaedheka au akaogopa﴾[2] na akasema aliyetukuka: ﴿Wala hatukukutumiliza ila ni rehma kwa viumbe wote﴾[3] na akasema aliyetukuka: ﴿Na wajadili kwa namna ambayo ni bora zaidi﴾ na kati ya hizo neno lake aliyetukuka: ﴿Na wazungumzieni wat wema﴾.

Na katika Hadithi tukufu ni kuwa Mtumi ﷺ baada watu wa twaif kumpiga majiwe malaika wa majabali alimaridhiya awafinike majabali juu yao Mtumi ﷺ akataa na akasema: (Hakika mimi nataraji Allah atowe kwenye migongo yao watakaomuabudu wala wasimshirikishe na yeye yoyote)[4].

Na katika vita vya Fathu Makkah Swahaba mmoja alisema: (Leo ni siku ya unyama) akasema ﷺ: (bali leo ni siku ya huruma) imepokewa na Ibn Asaakir na Waaqidiy na Amawiy katika vitabu vyao vya vita.

1 Muwaalaah ni kilma cha kiarabu kinachomaanisha kujikurubisha na mtu kiurafiki, na Mu'adaah ni kilma cha kiarabu kinachomaanisha kutangaza uaduwi.
2 Surat Twaha Ayah 43 - 45.
3 Surat-ul-Anbiyaa Ayah ya 107.
4 Hadithi hini imepokewa na Muslim.



Na Mtumi ﷺ alipoingiya Makkah akiwa ameifunguwa aliwakusanya maqureshi na akawaambiya: (Munadhani ni tawafanya nini?) wakasema: "Ndugu mkarimu na mtoto wa ndugu mkarim" akasema: (Nendeni kwani nyinyi muko huru)[1].

Na kwenye vita vya uhud walimvunja meno yake ya mbele na wakamtiya alama kichwa chake, na wakawauwa sabiini kati ya maswahaba zake, kati yao ni Hamza radhi za Allah juu yake, lakini yeye aliinuwa mikono akiomba na akisema: (Ewe Mungu wasamehe watu wangu kwani hakika wao hawajuwi)[2].

Na Mtumi ﷺ alipokwenda Madinah alifanya mkataba wa kupatana na mayahudi wa Madinah juu ya kuishi pamoja na kujiteteya kwa kushirikiyana, kama alivopokeya Abu Ubayd katika kitabu cha Al-Amwal na na Ibn Ishaaq katika Al-Maghazi, na mifano ya hayo kutokana na sera tukufu ni nyengi sana.

## Baadhi Ya Misimamo Ya Maswahaba Na Waliyotangulia Katika Kuamiliyana Na Wasiowaisilamu

Omar Ibn Khatwaab رضي الله عنه alipita mara moja kwenye mlango wa watu na kwenye mlango kulikuwa na yahudi yuwaomba huku akisema: "Mtu mzima kipofu wa macho" Omar akumuuliza: ni kitu gani kilichokufanya ufanye hivi? Akasema: "Ni haja na kulipa jizya[3]" Omar akamchukuwa mkono na akaenda naye nyumbani kwake na akampatia kitu kidogo kisha akatuma baruwa kwa mshika Beit-ul-Maal[4] na akamwambiya: "Muangaliye huyu na mfano wake, kwani wallahi itakuwa hatujamfanyiya usawa ikiwa tutakula ubarobaro wake kisha tumtupe wakati wa uzee, na akasoma neno lake aliyetukuka: ﴿Hakika swadaka ni za mafukara na masikini na wanaozifanyiya kazi na wanaozoweshwa nyoyo zao na kwa kukomboa shingo na wenye madeni na kwenye njiya ya Allah na mkatikiwa na njiya ni faradhi kutoka kwa Allah na Allah

1 Hadithi hini imepokewa na Bayhaqiy.
2 Hadithi hini imepokewa na Ibn Habaan kwenye Swahihi yake.
3 Jizya ni malipo wanayolazimika kulipa wasiowaisilamu wanapoishi chini ya himaya ya waisilamu.
4 Beit-ul-Maal ni bengi ama hazina ya mali ya dola ama nchi nzima.



Deviance_Isssue_07_Sw.indd 7 13/11/17 13:41

ni mjuzi mwenye hikma﴿[1] na akasema: (Mafukara ni waislamu na huyu ni katika masikini katika Ahl-ul-Kitaab[2] na ameondolewa jizya yeye na mfano wake) ameipokeya Abu yusuf katika kitabu chake Al-Kharaaj.

Na aliandika Khalid Bin Waliid kwenye mkataba wa dhimma[3] pamoja na watu wa Hira: (Mzee yoyote aliedhoofika na kazi au akapatwa na kasoro kutokana na kasoro au alikuwa tajiri akafukarika ikawa watu wanadini yake wanampatiya swadaka basi ataondolewa jizya yake na atasimamiwa yeye na anaowasimamiya kutokana na Beit-ul-Maal ya waislamu madamu anaishi kwenye ardhi ya Hijra na nchi ya kiislamu) piya imepokewa na Abu Yusuf katika chake Al-Kharaaj.

Na Omar bin Abd-ul-Aziz alimuandikiya Uday bin Artwah: (Na uangalie upande wako katika watu wa dhima aliyokuwa mkubwa umri wake, na zimedhuufika nguvu zake na ameondokewa na pato, basi mpatiye kutokana na Beit-il-Maal ya waislamu kinachomswilihi[4]) imepokewa na Abu Ubeid katika kitabu chake Al-Amwaal.

## Je Kuwapenda Wasiowaislamu Kwapingana Na Kujiepusha Na Ukafiri

Kupenda kwa muisilamu kwa asiomuisilamu ima iwe ni kwa ajili ya dini yake na ima ni kwa lengo lengine, hivo ikiwa ni kwa ajili ya dini yake basi huo ni ukafiri wenyewe, na ikiwa ni kwa lengo lengine basi ikiwa hilo lengo ni la haramu kishariya basi kupenda huko ni haramu kwa wakati huo, kama anaempenda kafiri wa kike kwa ajili anafanya haramu na yeye, lakini hili ni jambo inakuwa sawa pamoja na muisilamu na asiemuisilamu, hivo atakaempenda muislamu kwa kuwa anafanya na yeye haramu basi ni haramu, na ikiwa hilo lengo siharamu kama kuwa ni jamaa kwa mfano ama ni mwendani wake masomoni ama amemtekelezeya

1 Surat-ut-Tawbah Ayah ya 60.
2 Ahl-ul-Kitaab ni watu wote wanaofuata vitabu vilivoteremshwa na Allah ﷻ kama vile mayahudi.
3 Mkataba wa Dhimmah ni Mkataba wa amani unaopitishwa kati ya waisilamu na wasiowaisilamu.
4 Kwa maana kitakachomfaa na kumtosheleza mahitaji yake.



wema basi hakika kupenda kwake wakati huo kunanafaa, amesema Ibn Al-Wazeer katika kitabu chake Iythaar-ul-Haq alal-Khalq ukurasa wa (400): (Urafiki ulioharamishwa kwa Ijmaa' ni kumpenda Kafiri kwa ukafiri wake na Aaswi kwa maaswiya yake si kwa sababu ya kuvutiya manufaa au kujikinga na madhara au kwa ajili ya tabiya yake nzuri, na Allah ni mjuzi zaidi).

Na katika Iythaar-ul-Haq alal-Khalq piya (1/373): (Na kutokeya hapa wameijawizisha wanaobaniya kwenye Walaa' na Baraa' apendwe aswi kwa tabiya njema iliyoko ndani yake hata kama ni kafiri kama Abi Twalib katika moja wa kauli mbili, na kwa kauli nyengine ni kupendwa na Mtumi na jamaa zake kabla kusilimu).

**Na dalili juu ya kufaa kuwapenda wasiowaisilamu -sio kwa ajili ya dini yao- ni mambo yafuatayo:**

Mwanzo: Ni kuwa jambo hili ni la kimaumbile haiwezekani kujiepusha nalo, kwani kumpenda baba na mtoto na mwendani na anaefanya wema ni jambo la kimaumbile na kawaida . .
Pili: Neno lake aliyetukuka: ﴾Hakika wewe haumuogozi unayempenda lakini Allah anamuongoza anaemtaka﴿[1].

Hivo katika Ayah hini Allah aliyetukuka anatoa khabari kuhusu pendo la Mtumi wake ﷺ juu ya ami yake Abi Talib na kumtamaniya kwake uongofu pamoja na kuwa hakusilimu, hivo maana ya neno lake: ﴾unayempenda﴿ yani ambaye umempenda.

Tatu: Neno lake aliyetukuka: ﴾Na katika alama zake ni kuwa amewaumbiya nyinyi kutokana na nafsi zenu weke zenu ili mutuliye kwao na akajaaliya kati yenu upendo na huruma﴿[2].

Na katika kinachojulikana ni kuwa inafaa kumuowa Kitaabiyyah[3] Dhimiyyah[4] bali jamuhuri ya wanavyuoni wanaoneleya kufaa kumuowa Kitaabiyyah hata kama ni kati ya watu wa vita, kwa ujumla wa neno lake Allah aliyetukuka: ﴾Na waliojihifadhi kati

1 Surat-ul-Qaswas Ayah ya 56.
2 Surat-ur-Ruum Ayah ya 211.
3 Mwanamke kati ya Ahl-ul-Kitaab wale wanaofuata vitabu kama mayahudi na manaswara.
4 Dhimmiy ni kati ya Ahl-ud-Dhimmah wale wasiowaisilamu wenye mkataba wa amani na waislamu.



Deviance_Isssue_07_Sw.indd 8-9 13/11/17 13:41

ya waumini wa kike na waliojihifadhi kati ya wale ambao walipewa vitabu kabla yenu﴾[1].

Hivo basi hakuna neno kuweko ndani ya moyo wa muislamu upendo kwa mke wake ambaye ni Kitaabiyyah, bali hilo ni jambo la kimaumbile la kitabiya haiwezekani kuliondowa.

### Kuwazuru Wasiowaisilamu Na Kuwatembeleya Na Kuitikiya Uwalishi Wao Na Kuwataazii[2]

Imepokewa kutoka kwa Anas Allah awe radhi naye amesema: (Kulikuwa na kijana muyahudi akimtumikiya Mtumi ﷺ akawa mgonjwa Mtumi ﷺ akamjiya kumtembeleya, akakaa kwenye kichwa chake akamwambiya: "Silimu" akamuangaliya babake naye alikuwa kwake, akamwambiya: "Mtwii Abal-Qaasim" akasilimu, Mtumi ﷺ akatoka naye akisema: "Shukurani ni za Allah aliyemuokowa na moto")[3].
Na imepokewa kutoka kwa Anas رضي الله عنه : (Kuwa yahudi alimualika Mtumi ﷺ kula mkate wa nganu na mchuzi wa mafuta Mtumi ﷺ akamuitikiya)[4].

Na Ihalat Sunkhah ni mafuta ya mtuzi iliyobadilika harufu.
Na yameafikiyana madhehebu yote manne juu ya kufaa kumtaazii asiemuislamu.

### Kuwafanyiya Wema Wasiowaisilamu Na Kuwaunga Na Kupatiyana Nao Zawadi

Allah aliyetukuka amesema katika Qur'ani tukufu: ﴿Allah hawakatazi na wale ambao hawakuwapiga vita kwenye dini wala hawakuwatowa majumbani mwenu kuwatendeya wema na kuwafanyia usawa hakika Allah anapenda wanaofanya sawa (8) Hakika Allah anawakataza na wale waliyowapiga vita kwenye dini na wakawatowa kwenye majumba yenu na wakasaidia juu ya kutolewa kwenu; kuwafanya marafiki, na atakaewafanya marafiki basi hao ndio madhalimu﴾[5].

1 Surat-ul-Maaidah Ayah ya 51.
2 Kumtaazii mtu ni kumpatiya pole anapofiliwa na mtu wake.
3 Hadithi hini imepokewa na Bukhari.
4 Hadithi hini imepokewa na Imam Ahmad.
5 Surat-ul-Mumtahinah Ayah 8 - 9.



Imekuja katika sababu za kuteremka Ayah hini: Kutoka kwa Abdallah Ibn Zubeir رضي الله عنه amesema: "Iliteremka kuhusu Asmaa bint Abi Bakar, na alikuwa na mama kwenye Ujahiliya anaitwa Qatiyla bint Abd-ul-Uzza, akamjiliya na zawadi na Swinaab[1] na mkate wa maziwa na samli, akasema: " Sikubali zawadi yako, wala usiingiye kwangu mpaka Mtumi ﷺ atowe idhini" Aisha رضي الله عنها akalitaja hilo kwa Mtumi ﷺ ndio Allah ﷻ akateremsha: ﴿Allah hawakatazi na wale ambao hawakuwapiga vita kwenye dini ...﴾ imepokewa na Twabariy kwenye tafsiri yake.

Na katika Swahihi ya Bukhari kutoka kwa Asmaa رضي الله عنها alisema: "Mamangu amekuja naye ni mshirikina wakati wa mkataba wa mqureshi na muda wao walipoahidiana na Mtumi ﷺ pamoja na babake, nikamtaka fatwa Mtumi ﷺ nikasema: "Mamangu amekuja na anataka [kuunga kizazi] je nimuunge? Akasema: ( Ndio, muunge mamako).

Na kuna namna nyingi za wema na usawa na ihsani katika kuamiliyana na pamoja na wasiowaisilamu wasiovita zilizokusanywa na Ayah hini, na tutachukuwa yatakayokuwa mapesi kati yake kutokamana na vigawanyo vifuatavyo:

Kati ya hayo ni kupatiyana swadaka na zawadi na wao.
Imepokewa kutoka kwa Ibn Abbaas رضي الله عنه: (Kuwa Mtumi ﷺ baada kuteremka Ayah hini: ﴿Sio juu yako kuongokea kwao lakini Allah anamuongoza amtakae na munazotowa za kheri ni zenu wenyewe wala hamutowi ila ni kutaka radhi za Allah na munachotowa cha kheri mutalipwa na nyi hamutadhulumiwa﴾[2] aliamrisha kupewa swadaka kila aneomba kutoka kila dini) imepokewa na Ibn Abi Haatim katika tafsiri yake.

Na imepokewa kutoka kwa Said Ibn Al-Musayyib رضي الله عنه: (Kuwa Mtumi ﷺ alitowa swadaka kwa jamaa wa nyumba katika mayahudi, kwa hivo inapita juu yao" imepokewa na Abu Ubeid katika Al-Amwaal.
Na amepokeya Bukhari na Muslim رضي الله عنه : "Kuwa Omar ibn Khatwaab رضي الله عنه alimpatiya zawadi ya nguo ndugu yake mshirikina" Nawawi

1 Swinaab ni aina ya chakula.
2 Surat-ul-Baqarah Ayah ya 272.



Deviance_Isssue_07_Sw.indd 10-11 13/11/17 13:41

amesema katika sherehe yake juu ya Swahih Muslim (39/14) (Omar alimvalisha ndugu yake kwa mama mshirikina katika watu wa Makkah) na katika hili lote ni dalili ya kufaa kuwaunga kizazi makafiri na kuwafanyia hisani na kufaa kuwazawadi makafiri.

Na upande mwengine wengi kati wasiowaisilamu kutokana na wafalme na wengineo walimzawadi Mtumi ﷺ zawadi nyengi na akazikubali. Na kati ya hizo ni kukubali kwake zawadi za mfalme wa misri mkibtwi.

Imepokewa na Aisha رضي الله عنها alisema: (Mwenye skandariya[1] alimzawadi Mtumi ﷺ vijiti vya wanja vijiti viwili vya kishaam na kiyoo na kichana) imepokewa na Twabraniy katika Al-Awswat.

## Ujirani Mzuri

Na katika hayo ni ujirani mzuri na wao, Allah aliyetukuka asema: ﴿Na muabuduni Allah wala musimshirikishe na chochote na kwa wazazi wawili mufanye wema na kwa kizazi na mayatima na masikini na jirani mwenye ukaribu na jirani wa pambizoni na rafiki wa ubavuni na mpita njiya na waliomilikiwa na mikono yenu, hakika Allah hampendi ambaye ana kiburi anayejifakhiri﴾ [2].

Na anayekusudiwa kwa jirani wa pambizoni katika tafsiri zake mbili ni jirani asiomuislamu.

Kutoka kwa Nauf As-Shaamiy amesema: (Jirani mwenye ukaribu ni [kila] Muisilamu, na jirani wa pambizoni ni [kama] yahudi na naswara) kama ilivo kwenye tafsiri ya Twabariy.

Na imepokewa kutoka kwa Amru Ibn Shuaib kutoka kwa babake kutoka kwa babu yake kuwa Mtumi ﷺ amesema: (Majirani ni watatu, kati yao kuna wenye haki tatu na kati yao kuna wenye haki mbili na kati yao kuna mwenye haki moja, ama yule ambae ana haki tatu basi ni yule jirani, muisilamu na kizazi, ana haki ya uislamu na haki ya ujirani na haki ya kizazi, na ama yule mwenye haki mbili ni yule jirani muislamu, ana haki ya ujirani na haki ya uislamu, na ama yule mwenye haki moja basi ni yule jirani kafiri ana haki ya ujirani) imepokewa na Twabaraniy katika Musnad-us-Shaamiyyin na Bayhaqiy katika As-Shu'ub.

1 Skandariya ni mji uko Misrin, na ndio ulikuwa mji mkubwa wakati huo.

2 Surat-un-Nisaa Ayah ya 36.



Allah aliyetukuka amesema: ﴿Na saidiyaneni juu ya mema na uchajimungu wala musisaidiyane juu ya makosa na uaduwi na muogopeni Allah hakika Allah ni mwenye adhabu kali﴾ [1].

Mfumo wa Ayah hini ni dalili kuwa amri ya kusaidiyana juu ya mema na kutosaidiyana juu ya shari kwapatikana pamoja na wasiowaislamu piya, bali mfumo wake ni juu yao tangu mwanzo na hivo ndivo wamesema watu wa tafsiri.

Na Mtumi ﷺ alisema kuhusu Half-ul-Fudhuul Muungano walioupitisha makureshi katika zama za Jaahiliya kumnusuru aliyekuwa amedhulumiwa: (Nimehudhuriya katika nyumba ya Ibn Jadaan muungano si pendelei badili yake niwe na ngamia wekundu, na lau ningeitwa kuuhudhuriya katika zama za uisilamu ningeitikiya) imepokewa na Al-Humaydiy na At-Twahawiy.

Na akasema kuhusu Suluhu ya Hudaybiyah: (Lau makureshi wataniita kwenye mpangilio watakao tukuza ndani yake [mambo na sehemu] takatifu za Allah nigeitikiya)[2].

## Kuwasifu Wasiowaisilamu Na Kuwasifu Kwa Walionayo Ya Kheri

Baadhi ya watu wanadhaniya kuwa kumsifu asiomuislamu kwa aliyonayo ya kheri kunapingana na Al-Walaa' wa Al-Baraa' na hunu ni ufahamu wa makosa bila ya shaka mana Allah aliyetukuka asema: ﴿Wala yasiwapelekee nyinyi machukivu ya watu kwenye kutofanya uawadilifu, fanyeni uwadilifu hilo ni karibu zaidi na uchajimungu﴾ [3] na Ayah hini iko kwenye mpangilio wa kuzungumziya wasiowaislamu, bali Allah aliyetukuka amewasifu wasiowaislamu kwa ya kheri walionayo na vilevile Mja wake mtukufu ﷺ na hivohivo maswahaba رضي الله عنهم.

Na katika Ayah za Qur'ani katika hilo: ﴿Na utapata wenye pendo

1 Surat-ul-Maaidah Ayah ya 2.

2 Hadithi hini imepokewa na Bukhari.

3 Surat-ul-Maaidah Ayah ya 8.



Deviance_Isssue_07_Sw.indd 12-13 13/11/17 13:41

la karibu zaidi kwa wale walioamini ni wale waliosema sisi ni manaswara, hayo ni kwa kuwa kati yao kuna makasisi na maruhubani na hakika wao hawafanyi kiburi﴿[1] ﴾Hawako sawa kati ya Ahl-ul-Kitaab kuna ummah uliosimama wanasoma Ayah za Allah nyakati za usiku nao wanasujudu﴿[2] ﴾Na kati ya Ahl-ul-Kitaab kuna ambaye ukimuamini kwa mali mengi atakutekelezea kwako﴿[3].

Na katika Hadithi za Mtumi ﷺ katika hilo ni zile ambazo ni mashuhuri katika sera ya Mtumi ﷺ kuwa Mtumi ﷺ alipoona yanayowapata maswahaba wake makkah kutokana na balaa na kuwa hawezi kuwakomeshea yale waliyomo ndani yake, aliwambiya: (Lau mwatoka mukaenda ardhi ya habasha, mana hakika kuna mfalume hadhulumiwi kwake yoyote . . .) Kama ilivo kwenye Siyrat Ibn Hishaam (1/ 321).

Na alipokuwa ﷺ akituma baruwa kwa wafalume alikuwa akizianza kwa jina la kubandika wanalojulikana nalo hawo wafalume, hivo atasema [kwa mfano]: (Kwa jina la Allah mwenye kurehemu mwenye sikitiko, kutoka kwa Muhammad Mjumbe wa Allah kwenda kwa (Hiraql mkubwa wa ruum) (Kisraa mkubwa wa fursi) kama ilivyo kwenye hadithi swahihi katika kitabu cha Bukhari a Muslim, angalia mkusanyo kati ya swahihi mbili Bukhari na Muslim Juzuu (3/ 305).

Na katika yaliyopokewa kutoka kwa maswahaba ﵃ amepokeya Imam Ahmad katika Musnad yake (1/201) na (5/290) kutoka kwa Ummu Salamah ﵂ amesema: (Tuliposhukiya ardhi ya habasha, tulikuwa majirani huko na jirani bora An-Najaashiy alitupatiya amani juu ya dini yetu tukamuabudu Allah hatuudhiwi wala hatusikii kitu tunachochukiya, yalipowafikia hayo makureshi. . .).

Na katika Swahih Muslim (8/176) amesema Al-Mustawrid Al-Qurashiy mbele ya Amru Ibn Al-Aas: “Nimemsikiya Mjiumbe wa Allah ﷺ akisema: (Kitasimama kiyama na waruum ndio watu

1 Surat-ul-Maaidah Ayah ya 82.
2 Surat Aal Imraan Ayah ya 113.
3 Surat Aal Imraan Ayah ya 75.



wengi zaidi) Amru akamwambiya: “Angaliya unachosema!” akasema: “Nasema nilichokiskiya kutoka kwa Mjumbe wa Allah ﷺ” akamwambia: “basi kama umesema hivo, hakika wanayo mambo manne: Hakika wao ni watu wapole zaidi wakati wa fitna, na ni wepesi zaidi kuzinduka baada msiba, na ni wepesi zaidi kurudi baada kukimbiya, na ni wabora wa watu kwa masikini na yatima na dhaifu, na la tano ni zuri na la kupendeza: na wamekingika zaidi na dhulma za wafalume”).

### Shiri za maombolezi za Hassaan bin Thaabit kwa Al-Mutim bin Uday

Al-Mutim bin Uday alikufa kafiri, na pamoja na hilo Hassaan bin Thaabit ﵁ alisema: “Wallahi nitamuomboleza na hilo ni kwa kuwa yeye alimuhami Mtumi ﷺ wakati wa kurudi kwake kutoka twaaif” (Siyrat Ibn Hishaam na Fath-ul-Baari’ cha Al-Haafidh Ibn Hajar na Aalam-un-Nubalaa’ cha Al-Haafidh Ad-Dhahabiy na Al-Bidayah wa An-Nihayah cha Al-Mufassir Al-Haafidh Ibn Katheer) Akasema ndani yake:

*Ewe jicho hebu mliliye bwana wa watu, na umimine machozi na ukiyamaliza basi mimina damu*
*Na umliliye bwana na mkubwa wa tangao mbili mwenye zema kwa watu asiezungumza*
*Basi lau utukufu ungemweka mtu milele, utukufu wake leo ungembakisha Mut’im*
*Ulimuhami Mjumbe wa Allah wakawa watumwa kwako muda mwenye kuhirimiya kuitikiya*
*Hivo lau utamuuliziya makabila yote ya Maad na Qahtwan na waliobakia wa Jurhum*
*Wangesema yeye ndiye mtekelezi wa dhima na ahadi ya jirani yake iwapo atatukanika*
*Basi halitoki juwa la kun’gara juu yao kwa mfano wake kati yao mtukufu zaidi na mkarimu*
*Mzuizi akizuwiya na tabiya njema na mtulivu kwa jirani wakati usiku unapotanda kiza*



Deviance_Isssue_07_Sw.indd 14-15 13/11/17 13:41

## Kuwamakinisha Kusimamisha Tangao[1] Za Dini Yao Na Kufanya Yanayofaa Kwenye Dini Yao

Katika mambo ya kimsingi kwenye mkataba wa Ahlu-Dhimmah ni waisilamu wasiwaingiliye Ahlu-Dhimmah kwenye itikadi zao na tangao zao na kutekeleza ibada zao na sherehe zao na kazi zao ambazo wanazizingatiya ni katika mambo ya dini yao, kama kupiga maparapanda ndani ya sehemu zao za ibada, na kusoma taurati na injili bila kudhihirisha chochote katika hayo kati ya waislamu, kwa mana mkataba wa Ahlu-Dhimmah ni kuwakubaliya makafiri juu ya ukafiri wao kwa sharti ya kutowa Jizyah, na kuwa Ahlu-Dhimmah hawaingiliwi kwenye tangao zao, ni jambo limeafikianwa juu yake kati ya wanavyuoni, kwa ufafanuzi na tafauti kati yao kwenye baadhi ya sehemu. Kwa dhehebu la Hanafi angaliya: Hashiya ya Ibn Abideen (3/272) na kwa dhehebu la Maalik: Hashiya ya Ad-Dasuqiy (2/204) na dhehebu la Shafii: Mughni Al-Muhtaaj (4/257) na kwa dhehebu la Hanbal: Kashaaf Al-Qinaa' (3/133)

Piya wanavyuoni wameafikiyana kuwa Ahlu-Dhimmah wanakubaliwa waliyonayo ya nguruwe na tembo na vinanda na kula mchana wa ramadhani na majusi kuowa maharimu zao na mfano wa hayo kutokana na ambayo yafaa kwenye dini yao. Kwa dhehebu la Hanafi angaliya: Fath-ul-Qadiyr (5/300) na dhehebu la Shafii: Nihaayat Al-Muhtaaj (8/93) na kwa dhehebu la Maalik: Az-Zarqani juu ya Khalil (3/146) na kwa dhehebu la Hanbal: Kashaaf Al-Qinaa' (3/127)

Ila ni kuwa wanakataza kudhihirisha hayo kati ya waisilamu, na wanakataza kuwalisha waisilamu, na hilo ni kwa kuhifadhi salama ya kijamii, kama vile hali ya muisilamu asiefunga ndani ya ramadhani. Na mategemezi ya wanavyuoni katika yaliyotanguliya ni yale yaliopokewa kutoka kwa Mtumi ﷺ katika maafikiyano yake pamoja na manaswara wa najraan na mayahudi wa madina, na yaliyopokewa kutoka kwa maswahaba ﷺ ∑kutokana na maafikiyano yao pamoja na wasiowaisilamu walipokuwa wakifunguwa miji.

1 Tnagao za dini ni mambo ya kidini ambayo yaitangaziya dini na ni kama alama zake.



## Kuwaombeya Wasiowaisilamu

Katika Musannaf ya Ibn Abi Shaybah (8/457) amekusanya kitengo kuhusu yahudi na naswara anaeombewa, na amepokeya ndani yake hadithi kadhaa na yaliyopokewa, kati yake ni kutoka kwa Qatada ﷺ: (Kuwa yahudi mmoja alimkamuliya Mtumi ﷺ ngamiya akasema: (Ewe Mola mrembeshe) nyele zake zikawa nyeusi). Na imepokewa kutoka kwa Ibrahim alisema: "Alikuja yahudi kwa Mtumi ﷺ akamwambiya: "Niombee na mimi Mungu" akasema: (Allah ayafanye mengi mali yako na watoto wako na aupe swiha muili wako na aurefushe umri wako).

Na imepokewa kutoka kwa Ibrahim kuwa alisema: (Hakuna tatizo kumwambiya yahudi: Allah akuongoze).

Imepokewa kutoka kwa Said bin Jubeir kuwa amesema: (Lau firauni angeniambiya: "Allah akubariki" ningesema na wewe piya, na firauni amekufa).

Na imetanguliya kuwa Mtumi ﷺ aliwaombeya maqureshi kwenye vita vya uhud baada walipompasuwa, akasema: (Ewe Mola wasamehe watu wangu hakika wao hawajuwi).

Na alikuwa Mtumi ﷺ akimuombeya Abu Jahl na Omar kabla kusilimu kwake na akisema: (Ewe Mola utiliye nguvu uisilamu kwa anayempendeza zaidi kwako kati ya hawa watu wawili, Omar Ibn Khatwaab au kwa Abu Jahl Ibn Hishaam)[1].

Na mifano ya hilo kutoka kwenye Sunnah na maneno yaliyopokewa ni mengi sana, na katika tuliyoyataja yatosha.

1 Hadithi hini Imepokewa na Imam Ahmad na At-Tirmidhiy.



Deviance_Isssue_07_Sw.indd 16-17 13/11/17 13:41

## Kuweko Baadhi Ya Kuachiliya Katika Kuamiliyana Na Wasiowaisilamu Kwa Sababu. . . Je Kunapingana Na Kujiepusha Na Ukafiri?

Kuna matukio ya Mtumi ﷺ mengi alikuwa Mtumi ﷺ akiachiya ndani yake baadhi ya mambo kwa ajili ya maslaha ya kishariya katika siyasa, tutaje hapa matukio mawili peke yake:

Tukio la kwanza: Kilichotokea kwake ﷺ katika vita vya Ahzaab kutaka kuwaachia kabila la Ghatfaan thuluthi ya matunda ya madina kama badali ya kujiondowa kwao kwenye vita hivyo. Kama alivopokeya Ibn Abi Shaybah katika Muswannaf yake (14/420) na Abd-ur-Razzaaq kwenye Muswannaf yake (5/367)

Amesema As-Swaalihiy katika kitabu chake Subul-ul-Hudaa wa Ar-Rashaad (4/399): (Mtumi ﷺ amewapatiya dalili kwa kuorodhesha kwake kuwapatiya Ghatfaan thuluthi ya matunda ya madina, kufaa kumpatia aduwi mali ikiwa ndani ya hilo kunao maslaha ya waisilamu na akiba kwao).

Tukio la pili: Kilichotokea kwake ﷺ katika vita vya Al-Hudaybiyah kutokana na kuachia kwingi, kati yake ni kufuta (Bismillah) na kufuta kutaja kuwa yeye ni Mjumbe wa Allah, na kukubali kurudi kutoenda makkah na kutofanya umrah, na kukubali kwake kuwasalimisha waisilamu walioguria kwake na kuwarudisha kwa maqureshi, na kukubali kwake kutowarejesha watakaojiunga na washirikina kutokamana na waisilamu, na kwa kweli Mtumi ﷺ alimrudisha Aba Buswayr kwa washirikina alipoguria madina baada ya mafikiano ya Hudaybiyah, na hakumkubali Aba Jandal na alikuwa amekuja kwa hijra. Kama alivopokeya Bukhari kwenye Swahihi yake (2/974) katika kiswa kirefu cha Hudaybiyah.

Hapa ndipo mwisho wa mzunguko. . . Shukurani na sifa zote njema ni za Allah Mola wa viumbe wote na rehma na amani ziwe juu ya bwana wetu Muhammad na jamaa zake na swahaba zake na waliofuatiya.

*ʿAbd al-Fattāḥ bin Ṣālih Qudaysh al-Yāfiʿī*
*Yemen - Tarim*



الحمد لله رب العالمين

دار الفقيه للنشر والتوزيع
DAR AL FAQIH
PUBLICATION & DISTRIBUTION

visit our online bookshop at:
www.daralfaqih.com

سند
SANAD
www.sanad.network

Deviance_Isssue_07_Sw.indd 18-19 13/11/17 13:41

# MSURURU WA UPOTOFU NA UDANGANYIFU

Amesema Mjumbe wa Allah ﷺ: (Wataichukuwa hini elimu [Dini] waadilifu katika kila watakaokuja, watakaoiteteya kutokana na upotofu wa wenye kuzidisha na udanganyifu wa wenye kuharibu na ufafanuzi wa wajinga)[1]

Wamefahamu baadhi ya wenye fikra za makosa, maneno ya Allah Mtakatifu na Mtumi wake ﷺ kwa namna hailingani na mfumo wa kielimu uliopokewa kutoka kwa waliotangulia wema, wala kuchukuana na makusudio na misingi mikubwa ya ujumbe wa Mungu.Wakazichukua kusudi baadhi ya Ayah za Qur'ani tukufu ambazo ziliteremka kwa wasiowaisilamu wakaziteremsha kwa waisilamu, na wakachukua Ayah ambazo zimekuja si kwa jumla wakazifanya ni maagizo ya kwa jumla.Na wakapotosha maana ya maneno ya Allah na Hadithi za Mtumi wake mtukufu kwa namna imepelekea (kuweko) au kukita kwa ufahamu wa kimakosa sana ndani ya akili za waislamu wasiowasomi, uliowapelekea kwenye nyendo na vitendo havina ufungamano na dini ya unyenyekevu ya kiislamu. Tutajua kupitia msururu (mfululizo) hunu, upotoshaji wa maana ya maneno ya Allah na Mtumi wake, waliouangukia wenye fikra hizi za makosa, na kutilia nguvu kwao fahamu za makosa, kiasi kilichowafanya wawe kando na makusudiyo ya Allah na Mtumi wake na ufahamu wa wema waliotangulia.

1 Hadithi mash'huri ameiswahihisha Ibn Abd-il-Bar, na imepokewa kutoka kwa Ahmad bin Hanbal kua amesema: hiyo ni Hadithi swahihi.

دار الفقيه للنشر والتوزيع
DAR AL FAQIH
PUBLICATION & DISTRIBUTION

سند
SANAD

www.sanad.network
twitter: @sanadnetwork
facebook.com/sanadnetwork
youtube.com/sanadnetwork
instagram.com/sanadnetwork

Deviance_Isssue_07_Sw.indd 20 13/11/17 13:41